# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## KIKAO CHA AROBAINI NA NNE

**10 JUNI, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## KIKAO CHA AROBAINI NA NNE TAREHE 10 JUNI, 2024

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**564. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali inawasaidiaje Vijana wanaomaliza VETA na Vyuo vingine vya Ufundi kupata mitaji.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**565. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mkakati gani wa kuongeza Walimu wa Sayansi katika Shule za Sekondari Wilaya ya Meatu.

**566. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa Kituo cha Afya Igusule – Bukene.

**567. MHESHIMIWA KHADIJA SHAABAN TAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itashughulikia tatizo la upungufu wa Watumishi kwenye Vituo vya Afya na Zahanati nchini.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**568. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini Serikali itatunga Sheria kali ya kuzuia ukataji miti holela hasa kwenye maeneo yenye milima na miinuko ili kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.

**WIZARA YA FEDHA:**

**569. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa Wastaafu Mafao yao kwa wakati.

**570. MHESHIMIWA GEOFFREY IDELPHONCE MWAMBE (MASASI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kiasi gani Serikali inadaiwa na Wazabuni, Wafanyabishara, Wakandarasi na Walipa kodi kutokana na huduma, kazi na kodi zilizozidi.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**571. MHESHIMIWA DKT. ANGELINE SYLVESTER LUBALA MABULA (ILEMELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya kuweka taa katika Kiwanja cha Mpira cha CCM Kirumba - Mwanza.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**572. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Wananchi wa Mkoa wa Katavi wanapata hati za kumiliki ardhi.

**WIZARA YA UJENZI:**

**573. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa ujenzi wa vipande vya Barabara za lami kuunganisha Barabara Kuu na Reli ya SGR ili kurahisisha Wasafiri kufika Stesheni.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**574. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini TANAPA itamalizia ujenzi wa jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya Hunyari - Bunda.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**575. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itatumia Vyama vya Ushirika kuuza Nyavu za kuvua Samaki zenye viwango.

**576. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, upi mkakati wa Serikali kuhakikisha Wanyama wanapata chanjo ili kudhibiti magonjwa ya Wanyama.

## WIZARA YA AFYA:

**577. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itapeleka vifaa kwenye jengo jipya la Mama na Mtoto katika Hospitali ya META Mkoani Mbeya.

**DODOMA** **N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**10 JUNI, 2024** **KATIBU WA BUNGE**